# MTUMIAJI

Jarida la Mtumiaji

Juni 2025




## BAJETI 2025/26:
## WATUMIAJI KUNUFAIKA KUPITIA MFUMO WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

# JARIDA LA MTUMIAJI

## Yaliyomo


| | |
|---|---|
| TCRA-CCC | i |
| Dira na Dhamira | i |
| Majukumu ya Baraza | i |
| Manejimenti ya Baraza | i |
| Bajeti 2025/26: Watumiaji kunufaika kupitia mfumo wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 1 |
| Umuhimu wa usalama katika huduma za Posta, Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto | 2 |
| Sitapeliki, Kampeni ya kitaifa ya kupambana na utapeli wa mtandaoni | 3 |
| Watumiaji waelimishwa kuhusu matumizi sahihi na salama mtandaoni | 4 |
| Fahamu ulinzi wa taarifa binafsi kwa mtumiaji wa huduma za mawasiliano | 5 |
| Usalama wa Mtoto Mtandaoni | 6 |
| Dondoo Muhimu | 7 |
| Matukio katika picha | 8 |

# JARIDA LA MTUMIAJI

## TCRA-CCC

TCRA CCC ni Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano ni chombo kilichoundwa kisheria chini ya Kifungu cha 37 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Na. 12 ya mwaka 2003 kwa madhumuni ya kulinda na kutetea maslahi na haki za mtumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano Tanzania katika nyanja za:-

- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
- Utangazaji
- Huduma za Posta, Vifurushi na Vipeto

## MAJUKUMU YA BARAZA

**1.** Kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano zinazosimamiwa kisheria kwa kushauriana na Mamlaka, Waziri mwenye dhamana ya mawasiliano, na mawaziri wa sekta.

**2.** Kupokea na kusambaza taarifa na maoni kuhusu masuala ya msingi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano.

**3.** Kuanzisha kamati za watumiaji katika ngazi za mikoa, wilaya na sekta na kushauriana na kamati hizo.

**4.** Kufanya mashauriano na wahusika katika sekta, serikali na makundi mengine ya watumiaji wa huduma kuhusiana na masuala ya msingi ya watumiaji wa huduma zinazosimamiwa kisheria.

## BODI YA WAHARIRI

**Mwenyekiti :** Bi. Mary Shao Msuya
**Katibu :** Bw. Hilary Tesha
**Mwandishi :** Bw. Thomas Paul Kibaja

**Anwani ya ofisi za uhariri**
14 Mtaa wa Jamuhuri,
Postikodi 1516/ 11470 Dar es salaam
Barua pepe:barua@tcra-ccc.go.tz
Simu: +255(0) 22212269 / +255 652 966 633

## DIRA NA DHAMIRA

### DHAMIRA

Kutetea haki za watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano zinazosimamiwa kisheria kwa kuwawezesha watumiaji, uraghibishi, na mazungumzo na wadau.

### DIRA

Kuwa taasisi yenye ufanisi katika utetezi wa kulinda haki na maslahi ya watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano zinazosimamiwa kisheria nchini.

## MENEJIMENTI



**KATIBU MTENDAJI**
**Bi. Mary Shao Msuya**



**Mkuu wa Idara ya Fedha na Utawala**
**CPA. Formela B. Kanyika**



**Mkuu wa Idara ya Elimu na Uhamasishaji**
**Bw. Hilary Tesha**

# BAJETI 2025/26:
# WATUMIAJI KUNUFAIKA KUPITIA MFUMO WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

**Dodoma.** Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa, Mei 16, 2025 aliwasilisha Bungeni bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/26, akisisitiza mpango wa Serikali wa kuimarisha mfumo wa mawasiliano wenye kuendeleza Watumiaji kupitia uchumi wa kidijitali nchini.



*Katika picha ni Mhe Jerry William Silaa (Mb.), akitoa hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/26 ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliyowasilishwa bungeni*

Katika hotuba yake, Waziri Silaa alieleza kuwa Wizara imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 291.5, ambapo shilingi bilioni 277.0 zitatumika kwa miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa minara 758 katika kata 713, na kuunganisha wilaya 11 na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Bajeti hiyo itasaidia kuboresha mazingira ya biashara mtandaoni kupitia kuhakiki taarifa za anwani za makazi katika halmashauri 28 na kusimamia uundaji wa mfumo wa kidigitali wa biashara mtandaoni.

Aidha, Mfumo wa kidigitali wa biashara mtandaoni nchini Tanzania ni njia ya kisasa ya kuendesha biashara kwa kutumia teknolojia ya habari na Mawasiliano kwa kupitia vifaa vya kidigitali kama kompyuta, simu janja, na programu maalum kuhusisha shughuli za kibiashara kama vile kuuza na kununua bidhaa au huduma kupitia tovuti, mitandao ya kijamii, au majukwaa ya e-commerce kama Duka Mtandao la Posta Tanzania (**kipepeoshop.co.tz**) au WhatsApp Business, Facebook na Instagram.

Sambamba na hayo, kupitia uboreshwaji wa Anwani za makazi Watumiaji wa huduma za Mawasiliano nchini wataweza kutumiwa bidhaa zao walizonunua bila kupotea kwa kupitia huduma za posta hivyo kusaidia kuchochea maendeleo ya kibiashara na jamii kwa ujumla.

Bajeti hii inalenga kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara Mtandaoni na kuboresha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali hivyo kuchochea ajira mpya na kukuza kipato kwa watumiaji wa huduma za Mawasiliano nchini.

***Kwa taarifa zaidi, bofya HAPA***

## FAHAMU KUWA

**Mfumo huu unaleta mapinduzi ya kisasa katika uendeshaji wa biashara kwa kuongeza ufanisi unaoendana na mabadiliko ya kiteknolojia, kupunguza gharama, na kufungua fursa mpya za ajira na masoko, hususan kwa vijana na wafanyabiashara wadogo.**

**Serikali ya Tanzania inaendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na mifumo ya biashara mtandaoni, ili kuwawezesha Watumiaji hasa wafanyabiashara kuweza kufikisha bidhaa au huduma kwa wateja wao kwa haraka, usalama, na kwa ufanisi zaidi.**



CHANZO: Shirika la Posta Tanzania

## UMUHIMU WA USALAMA KATIKA HUDUMA ZA POSTA, USAFIRISHAJI WA VIFURUSHI NA VIPETO

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC) katika kuelimisha umma linawahimiza Watumiaji wa huduma za Mawasiliano nchini, kuzingatia usalama wanapotumia huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi pamoja na vipeto ili kulinda mali zao na kuepuka hasara zisizo za lazima.

Huduma za posta nchini Tanzania zipo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, huku uratibu wa shughuli za kila siku ukitekelezwa na Shirika la Posta Tanzania. **Huduma hizi zinajumuisha usafirishaji wa barua za kawaida, vipeto, vifurushi, pamoja na huduma mahsusi kama Posta Mlangoni, nyaraka kwa wasioona, Post Cargo na M-Bag.**

Katika siku za hivi karibuni kutokana na ukuaji wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari nchini, huduma hizi zimekuwa mkombozi kwa wananchi na wafanyabiashara, hasa kutokana na kuongezeka kwa biashara za mtandaoni.

Mtumiaji wa huduma za Posta nchini, kwa kazi binafsi au za kibiashara anaweza kununua, kuuza kwa kupitia mitandao ya kijamii au tovuti za biashara na kusafirisha mizigo ndani na nje ya nchi kwa kutumia Shirika la Posta au watoa huduma waliothibitishwa na TCRA.

Kwa upande wa ndani ya nchi, mizigo hufikishwa moja kwa moja hadi nyumbani au ofisini kupitia Anwani ya Makazi na Postikodi kwa usalama zaidi.

Aidha, kutokana na takwimu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika **"Ripoti ya Takwimu ya Sekta ya Mawasiliano ya Robo ya mwaka inayoishia Juni 2025"** inaonesha kuwa, Mgawanyo wa bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi ni 45% ikilinganishwa na 55% ya bidhaa zilizopokelewa nchini kupitia huduma za Posta.

Hata hivyo, changamoto zimeanza kujitokeza baada ya baadhi ya Watumaji wa huduma hizi kutumia watoa huduma/mawakala wa usafirishaji wasiosajiliwa. Hii wakati mwingine endapo kunatokea upotevu katika usafirishaji, kupelekea mtumaji kukosa kulipwa fidia.

Ili kuepuka madhara hayo, watumiaji wanashauriwa kutumia huduma rasmi za posta au kampuni zenye leseni kutoka TCRA. Hii ni njia salama katika biashara, kulinda taarifa binafsi na kuongeza uaminifu kwa wateja wao.

### KUMBUKA



**Kufunga kifurushi chako vizuri kwa usalama wako na hakikisha kina maelezo sahihi ya mtumaji na mpokeaji kama (jina, anwani kamili, namba ya simu, maelezo ya mzigo na thamani yake).**




**Tembelea ofisi ya Posta au watoa huduma wenye leseni kutoka TCRA, hakikisha kujaza taarifa zilizo sahihi na hii itakusaidia kama kunachangamoto yoyote kuweza kulipwa fidia.**



**Lipa gharama kutegemeana na thamani ya kifurushi, uzito, ukubwa, umbali wa kusafirishwa na hakikisha kupata risiti kama uthibitisho wa usafirishaji na yenye taarifa zote muhimu na namba ya ufuatiliaji.**

## SITAPELIKI:
## KAMPENI YA KITAIFA YA KUPAMBANA NA UTAPELI WA MTANDAONI

**Arusha.** Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa (Mb.), tarehe 20 Februari, 2025 alizindua rasmi kampeni ya kitaifa ya elimu kwa umma dhidi ya utapeli wa mtandaoni, inayojulikana kama "SITAPELIKI". Kwa lengo kuelimisha umma jinsi ya kuepuka utapeli na kuwa salama mitandaoni.




*Katika picha, wa pili kushoto ni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa (Mb.) akizindua kampeni ya **"SITAPELIKI"** wakati wa kikao kazi cha Serikali na wadau wa Sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali (2024 – 2034) katika ukumbi wa Jengo la PAPU jijini Arusha.*

Kampeni hii inalenga kuwaelimisha Watanzania, hususan watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano, kuhusu mbinu mbalimbali zinazotumiwa na matapeli wa mtandaoni, pamoja na kuwahimiza kuchukua tahadhari mahususi za kujilinda ili kuwa salama Mtandaoni.

Aidha, katika kuchukua tahadhari na kujilinda dhidi ya utapeli, Mtumiaji anapaswa kuhakikisha kutumia nywila thabiti na tofauti kwa kila akaunti mtandaoni, kutokubofya viunganishi (link) bila kujua vyanzo vyake, kutotekeleza maelekezo ya kutuma pesa au taarifa binafsi bila kuthibitisha muhusika anayemtumia.

Vile vile, Mtumiaji anapaswa kuwasiliana na mtoa huduma wake kwa kupitia namba 100 pekee na kuripoti majaribio ya utapeli kwenda namba 15040, pamoja na kuhakiki usajili wa laini za simu kwa kupitia namba *106#.

Kampeni hii ilikutanisha wadau mbalimbali wakiwemo watumiaji, watoa huduma za mawasiliano, na wadau wengine muhimu katika sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kama sehemu ya ushirikiano na juhudi za pamoja za kukabiliana na wimbi la vitendo vya utapeli mtandaoni dhidi ya watumiaji nchini.

Ushirikiano huu umeweza kuzaa matunda katika nchi, kwani kutokana na takwimu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika **"Ripoti ya Takwimu ya Sekta ya Mawasiliano - Robo ya mwaka inayoishia Juni 2025,"** inaonesha majaribio ya ulaghai kwa ujumla yamepungua kwa wastani wa **19%**.

| Robo ya mwaka inayoishia | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Machi 2025 | 5,876 | 1,724 | 2,484 | 3,925 | 3,143 | 17,152 |
| Juni 2025 | 2,595 | 2,882 | 2,478 | 1,658 | 4,224 | 13,837 |
| Badiliko | -56% | 67% | -0.2% | -58% | 34% | -19% |

## WATUMIAJI WAELIMISHWA KUHUSU MATUMIZI SAHIHI NA SALAMA MTANDAONI

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC) limeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuelimisha na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini kwa kutoa elimu inayowasaidia katika matumizi sahihi na salama mtandaoni.

Aidha, Baraza kupitia Kamati za Watumiaji za mikoa mbalimbali nchini, limekuwa mstari wa mbele katika kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini kuhusu matumizi sahihi na salama mtandaoni.



*Katika picha ni Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Mkoa wa Simiyu, Bw. David Wambura, akitoa elimu juu ya* ***Matumizi Sahihi ya Huduma za Mawasiliano*** *katika Shule ya Sekondari Biashara, iliyopo Kata ya Sima, Halmashauri ya Mji wa Bariadi – mkoani Simiyu. Jumla ya wanafunzi 1,620 pamoja na walimu 24 walihudhuria.*

Elimu hiyo inalenga kusaidia jamii kujiepusha na changamoto zinazojitokeza katika mazingira ya kidijitali kama vile **utapeli wa mtandaoni, unyanyasaji, jumbe za uongo, uchochezi, ulinzi wa taarifa binafsi, pamoja na usalama wa watoto mtandaoni.**

Juhudi hizi zinafanyika kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), pamoja na wadau mbalimbali wa sekta ya mawasiliano, ikiwa ni sehemu ya dhamira ya pamoja ya kuhakikisha kuwa haki na usalama wa mtumiaji wa huduma za mawasiliano unalindwa ipasavyo.

Mnamo Februari 20, 2025, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa (Mb.), alizindua rasmi kampeni ya kitaifa ya "SITAPELIKI" inayolenga kukabiliana na uhalifu wa mtandaoni na kuhimiza tahadhari miongoni mwa watumiaji wa huduma za mawasiliano, hasa katika matumizi ya simu za mkononi na intaneti.

Katika kuunga mkono kampeni hiyo, Katibu Mtendaji wa TCRA-CCC, Bi. Mary Shao Msuya, Machi 10, 2025 katika kipindi cha Kumepambazuka na Redio One. Amewahimiza watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini kuchukua tahadhari kwa kutumia nywila imara, salama na tofauti kwa kila akaunti katika mitandao; kuepuka kubofya viunganishi wasivyokuwa na uhakika navyo; na kutotoa taarifa binafsi bila kujiridhisha na uhalali wa chanzo au mtu anayezihitaji.

Sambamba na hayo, Watumiaji wanakumbushwa kuwasiliana na watoa huduma kupitia namba 100 pekee, kuripoti utapeli kupitia namba 15040, na kuhakiki usajili wa laini zao kwa kupiga *106#.

### MUHIMU

**Piga *106# kuhakiki usajili wa laini zilizosajiliwa kwa kitambulisho chako cha NIDA na iwapo utabaini namba usiyoifahamu, toa taarifa kwa mtoa huduma wako ili kuifuta.**

**Sifa ya nywila (Password) imara na salama , inapaswa kuwa na mchanganyiko wa herufi kubwa, ndogo, alama na namba.**

**Mtumiaji wa huduma za mawasiliano, unashauriwa kulinda taarifa zako kwa kutokuzitoa kwa Taasisi ambazo hazijasajiliwa nchini na Tume ya Ulinzi wa Taarifa binafsi .**

**Kabla ya kufanya malipo au kununua bidhaa mtandaoni, hakikisha tovuti uliyoichagua inatumia itifaki salama ya Mawasiliano (HTTPS).**

# FAHAMU ULINZI WA TAARIFA BINAFSI KWA MTUMIAJI WA HUDUMA NA BIDHAA ZA MAWASILIANO

Katika zama hizi za maendeleo ya Mawasiliano na teknolojia ya habari nchini, matumizi ya bidhaa na huduma za mawasiliano yamekuwa sehemu muhimu ya maisha ya kila siku kwa Watanzania. Hata hivyo, matumizi haya huambatana na changamoto ya uvujaji wa taarifa binafsi. Lakini je, unafahamu nini maana ya taarifa binafsi?

Taarifa binafsi ni maelezo yoyote yanayoweza kumtambulisha mtu, kama vile jina, namba ya simu, anwani, barua pepe, namba ya NIDA, taarifa za benki, afya, picha/video binafsi, au alama za vidole na Watumiaji wengi wanatoa taarifa hizi pasipo kuwa na ufahamu wa kutosha na namna zitakavyoenda kutumika, kama kwenye mitandao, hoteli, huduma za mikopo na sehemu nyingine mbalimbali.

Kwa kutambua umuhimu wa kulinda taarifa hizi, tarehe 3 Aprili 2024, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alizindua rasmi Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kwa mujibu wa Sheria Na. 11 ya mwaka 2022. Tume hii inasimamia usajili wa taasisi, upokeaji wa malalamiko, na kulinda faragha ya wananchi



*katika picha ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi katika Kituo cha Mikutano ya Kimataifa ya Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam 03 Aprili, 2024.*

Aidha, katika sehemu ya mwendelezo wa utoaji elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na Kamati za Watumiaji za mikoa kuhusu **Usalama Mtandaoni na Ulinzi wa Taarifa Binafsi**, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC) limetoa ushauri kwa Watumiaji kuhakikisha taasisi au makampuni wanayowapa taarifa zao binafsi kuwa..

..yamesajiliwa rasmi na PDPC kwani kufanya hivyo itamsaidia kuongeza usalama na kulinda taarifa zao.

Akizungumza kwenye kipindi cha Bonanza cha Radio Free Africa tarehe 6 Machi 2025, Mkuu wa Idara ya Elimu na Uhamasishaji ya TCRA-CCC. Bw. Hilary Tesha, alisisitiza kuwa "Mtumiaji ana haki ya kufahamu sababu ya ukusanyaji wa taarifa zake, kupata nakala, kuzifuta au kuzuia kuchakatwa na kulalamika ikiwa faragha itavunjwa na taasisi au makampuni."

## KUMBUKA

**Ulinzi na usalama wa taarifa zako binafsi unaanza na wewe.**


**Fahamu matumizi ya taarifa zako kabla ya kuzitoa.**

**Unaweza kuzuia kuchakatwa kwa taarifa zako na kulalamika ikiwa faragha itavunjwa.**

## USALAMA WA MTOTO MTANDAONI

Katika ulimwengu wa sasa, matumizi ya mitandao yamekuwa sehemu ya maisha ya kila siku kwa watoto wengi nchini Tanzania. Lakini je, sisi kama wazazi au walezi tunachukua hatua stahiki kuhakikisha usalama wao wanapotumia mtandao?

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kupitia kitabu cha **"Kuwa Salama Mtandaoni"** kilichochapishwa Oktoba 2022, takribani asilimia 67 ya watoto wenye umri wa miaka 12 hadi 17 hutumia mtandao kwa shughuli mbalimbali kama kujielimisha, kuburudika na kuwasiliana.




Hii inamaana kuwa, kati ya kila watoto 10. Watoto 7 tayari wanatumia mtandao na ni watoto 3 pekee wasio na uhusiano wa moja kwa moja na mitandao.

Ingawa teknolojia imefungua fursa nyingi chanya kwa watoto, changamoto zinazowakabili mitandaoni pia ni kubwa. **Bila usimamizi mzuri, watoto hujikuta wakikumbana na hatari kama unyanyasaji mtandaoni, udanganyifu kutoka kwa wahalifu, pamoja na kuingizwa kwenye mahusiano hatarishi na mafataki wa mtandaoni.**




*Katika picha ni Kamati ya Watumiaji Mkoa wa Kaskazini Unguja, baada ya kutoa elimu ya **Usalama wa Mtoto Mtandaoni** pamoja na **Haki na Wajibu wa Mtumiaji wa huduma za Mawasiliano** kwa wazazi na walezi katika kitongoji cha Chaani Mcheza Shauri, 06 Aprili, 2025.*

Vilevile, watoto hukutana na picha zisizofaa, taarifa za uongo, na hata kuathirika na uraibu wa michezo ya mtandaoni au matumizi kupita kiasi ya mitandao ya kijamii, hali inayoweza kudhoofisha maendeleo yao kielimu na kiakili.

### WAJIBU WA KILA MZAZI NA MLEZI

1. **Kutumia mifumo ya kuchuja taarifa (parental control).**
2. **Kuwapa elimu sahihi ya matumizi salama ya mtandao.**
3. **Kuwasimamia muda na aina ya maudhui wanayoangalia mtandaoni.**
4. **kuwasikiliza, kuwaongoza na kuwasaidia watoto wanapokumbana na changamoto za kidijitali.**



*Katika picha ni Kamati ya Watumiaji Mkoa wa Iringa, ikitoa elimu ya **Usalama wa Mtoto Mtandaoni** tarehe 29 Mei, 2025 katika Shule ya Sekondari Shabaha, iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa. Jumla ya wanafunzi 663 walihudhuria mafunzo hayo, wakiwemo wavulana 325 na wasichana 338.*

# DONDOO MUHIMU

## JE, WAJUA?

- **Barua za Kawaida:** ni barua zisizozidi uzito wa kilogramu mbili (2kg) na kwenda ndani na nje ya nchi.
- **Rejesta:** ni barua yenye uzito wa kilogramu mbili (2kgs) na lazima iwekwe namba maalum ya ufuatiliaji (tracking number) na huashiria kuwekwa vitu vya thamani ndani yake kama hati, vyeti, nk.
- **Vipeto:** ni tofauti na barua za kawaida kwa kuwa huwa na vitu vya thamani ndani mwake na kufungwa kama kifurushi kidogo chini ya kilo tatu (3Kgs). Huwekwa namba maalum ya ufuatiliaji (tracking number) kwa mtiririko wa vipeto.
- **Vifurushi vya kawaida:** hivi huanzia uzito unaozidi kilo 3 hadi kilo 30 na huwekwa namba maalum ya ufuatiliaji (tracking number) kwa vifurushi vya nchini na vya kimataifa. Vifurushi vya kimataifa lazima vifungwe mbele ya afisa wa Posta na maafisa Ushuru wa Forodha ili kuorodhesha kwa uhakika vitu vilivyofungwa ndani ya kifurushi.
- **Posta Mlangoni:** Hii ni huduma ya kupeleka nyaraka na vifurushi kutoka ndani na nje ya nchi, moja kwa moja hadi nyumbani au ofisini, kulingana na Anwani ya Makazi na Postikodi ya mteja.

## FAHAMU VIPAUMBELE VYA BAJETI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA 2025/26

- Kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa miongozo inayosimamia Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.
- Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na Posta kote nchini.
- Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara mtandaoni nchini.
- Kuimarisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali.
- Kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao.
- Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni changa (Startups).

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA MATUMIZI SAHIHI YA MTANDAONI

- Usalama Mtandaoni unaanza na wewe.
- Epuka kuweka taarifa zako binafsi zisizo na umuhimu mtandaoni.
- Sambaza taarifa zenye ukweli na uhakika.
- Tumia vyanzo rasmi vya habari kuhakiki taarifa kabla ya kuiamini na kuisambaza kwa wengine.
- Futa ujumbe wa uongo, matusi, au taharuki /uchochezi wa kuleta vurugu katika jamii.
- Kuwa sehemu ya kuhamasisha matumizi sahihi na salama mtandaoni.
- Shiriki kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu taarifa zisizo sahihi mitandaoni.

# MATUKIO KATIKA PICHA



**Dodoma.** Kushoto ni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa (Mb.), akipongezana na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi, mara baada ya kupitishwa kwa **Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026,** Bungeni jijini Dodoma. 16 Mei, 2025.



CHANZO: Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

**Dar es salaam.** Baadhi ya viongozi kutoka sekta ya umma na binafsi, pamoja na wadau na wageni waalikwa wa **Mkutano wa 14 wa Jukwaa la Afrika la Utawala wa Mtandao (AfIGF 2025),** wakifuatilia hafla ya ufunguzi wa mkutano huo iliyofanyika tarehe 30 Mei 2025, katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam, Tanzania. Ufunguzi huo ulifanywa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa (hayupo pichani).



**Manyara.** Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Mkoa wa Manyara ikitoa elimu ya **Haki na Wajibu wa Mtumiaji pamoja na Usalama Mtandaoni** kwa wanafunzi wa chuo cha Manyara Institute of Health & Allied Sciences (MIHASS) ili kuweza kuwasaidia katika changamoto mbalimbali za kimtandao. 28 Juni, 2025.




**Kigoma.** Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Mkoa wa Kigoma imetoa elimu ya **Matumizi Sahihi ya Huduma za Mawasiliano na Usalama Mtandaoni** kwa Watumiaji kupitia Radio Main FM 97.1, lengo likiwa ni kuongeza uelewa wa watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini. 08 Januari, 2025.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano
(TCRA CCC)
14 Jamhuri Street,
P.O.BOX 1516, 11470 DAR ES SALAAM
barua@tcra-ccc.go.tz
+255(0)22212269/+255 652 966 633